

TANGAZO LA NAFASI MBALIMBALI ZA MASOMO.

Chuo Kikuu cha Maastricht kilichopo Uholanzi kinatoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi kutoka mataifa yanayoendelea wanaotaka kujiunga na chuo hicho.

Ufadhili huu ni kwa wale wanaotaka kujiendeleza na Shahada ya Uzamili katika kozi mbalimbali zinatolewa chuoni hapo.

Masharti

- Mwombaji hatakiwi kuwa na uraia wa nchi yoyote iliyo chini ya jumuiya ya Ulaya
- Mwombaji anatakiwa awe ametimiza vigezo vya kujiunga na chuo kikuu cha Maastricht kabla ya kuomba ufadhili.
- Mwombaji hatakiwi kuwa amepitia ngazi yoyote ya elimu nchini Uholanzi.
- Umri usizidi miaka 35.
- Waombaji wenye ufaulu mkubwa watapewa kipaumbele.

Tuma maombi kupitia tovuti hii <https://www.maastrichtuniversity.nl/support/your-studies-begin/coming-maastricht-university-abroad/um-scholarships-students-abroad>

Mwisho wa maombi ni Februari 1, 2018

Serikali ya Sweden inatoa jumla ya nafasi 180 za ufadhili kwa wanafunzi wanaotaka kujiunga na vyuo vikuu mbalimbali nchini humo. Ufadhili huu ni kwa kozi zote za Shahada ya Uzamili zinazotolewa na chuo husika ambacho mwombaji atafanikiwa kupata nafasi.

Masharti

- Mwombaji anatakiwa awe na uzoefu wa kufanya kazi. Hii haitajalisha iwe ya kuajiriwa kujijiri au kujitolea.

Mwisho wa kutuma maombi ni Januari, 15 2018.

Chuo Kikuu cha Sydney kilichopo Australia kinatoa nafasi za ufadhili kwa wanaotaka kujiendeleza na Shahada ya Uzamili na Uzamivu.

Masharti

- Lugha ya kiingereza ni kigezo muhimu kwa waombaji.
- Waombaji wenye ufaulu mkubwa watapewa kipao mbelr.

- Mwombaji anatakiwa aandike insha ya maneno 1000 akieleza kwa nii apewe ufadhili huo.

Tuma maombi kupitia tovuti hii

<http://sydney.edu.au/scholarships/prospective/international-postgraduate-scholarships.shtml#usi>

Mwisho wa kutuma maombi ni Machi, 2018

Chuo Kikuu cha Radboud kilichopo Nchini Uholanzi kinatoa nafasi za ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wanaotaka kujiunga na Chuo hicho.

Nafasi 30 ziko wazi kwa ajili ya waombaji wa ufadhili huo ukiwalenga zaidi wanafunzi kutoka mataifa yanayoendelea.

Ufadhili huo uko katika vitivo vya sayansi, matibabu, sheria, filosofi, thiolojia na masomo ya dini, sayansi ya jamii na sheria.

Masharti

- Mwombaji hatakiwi kuwa na uraia wa nchi yoyote ya Ulaya
- Mwanafunzi aliyepata shahada ya kwanza Uholanzi hatakiwi kuomba ufadhili.

Tuma maombi kupitia tovuti hii

<http://www.ru.nl/english/education/master's-programmes/financial-matters/scholarships-grants/read-more/rsprogramme/>

Mwisho wa tuma maombi ni Machi, 18 2018.